TANGAZO LA SERIKALI NA. 377 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO, MINADA NA MAGULIO (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2020

Jina la sheria

Tangazo la Serikali Na 101 la Mwaka 2011

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Minada na Magulio (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Minada na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2011, ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama "Sheria Ndogo Kuu"

Marekebisho ya kifungu cha 8

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 8 na badala yake kuweka kifungu kipya cha 8 kifuatacho:

"8. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja."

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la madiwani ulioitishwa tarehe 15/5/2018.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*